NM
Jarida la kifasihi

# NGURUMO ya MWANDISHI

Toleo La XIII
Oktoba - MMXXII



## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Mwaka Mmoja Tumenguruma—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Julie Mmassi— Uk 03

**NEW IN TOWN**— 20 Kali za Ninja Kaisal Ally— Uk 04

Maonesho ya Vitabu ya Kimataifa— Uk 04

**PITIO LA VITABU**— Mwimbula— Uk 05

**MAKALA**— Safari ya Ngurumo ya Mwandishi— Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Usiwe Muuaji— uk 08 na 09

**HADITHI FUPI:** Tabia— Uk 10

**ANA KWA ANA**: Abigael Mwafulilwa: Muuza Maziwa Msoma Vitabu—Uk 11

**RIWAYA:** Mpigambio—Uk 12 na 13

**MATANGAZO:** Uk 14

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**MHARIRI: RICHARD MWAMBE**

**MSAIDIZI: REY STANLEY**

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

**WhatsApp: +255 734 550 514**

## TAHARIRI: Mwaka Mmoja Tumenguruma

Amani iwe kwenu,

Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha leo hii ambapo jarida letu la Ngurumo ya Mwandishi linatimiza mwaka mmoja. Mwaka mmoja tumenguruma na kutoa mafichoni kila kilichotakiwa kutoka na kazi inaendelea.

Kwanza kabisa nitoe pole sana kwa wote waliofikwa na msiba mzito wa ndugu, jamaa, na marafiki waliopoteza maisha kwenye ajali ya ndege iliyotokea huko Kagera mapema mwezi wa huu!

Tunashukuru kwa watu waliokuwa wa kwanza kujitolea kuweka rehani maisha yao kuwaokoa manusura wa ajali hiyo. Hakika ilikuwa ushujaa mkubwa na wanastahili tuzo.

Ninarudia na nitarudia kuandika na kuiambia serikali, majanga hayana mwenyewe. Kwanini tusiwekeze kwenye idara za uokoaji kwa kuwapa vifaa vya kisasa kuanzia vya mawasiliano mpaka vya wokozi ili kupunguza vifo visivyo vya lazima? Tunakwama wapi?

Kwanini siasa tunaziweka kwenye uhai wa watu? Tazama vifo vya watu kumi na tisa, wataalam kwenye kada mbalimbali ziwe za serikali au za binafsi, ambao kwa namna moja au nyingine walikuwa katika majukumu yao kikazi. Wapo watoto wamebaki bila mama au bila baba, wapo waume wamebaki wagane na wake waliobaki wajane.

Ajali haina kinga, ni sahihi. Na wala haijulikani wakati na saa ngapi itatokea, lakini tufundishike.

Tunaiomba serikali iongeze nguvu, itenge bajeti ya kutosha katika kuwezesha idara za uokoaji, kuzipatia vifaa na mafunzo kazi ili wafanye mambo kwa weledi. Waongeze ajira kwa vijana, tuna vijana wengi wanaoweza kumudu kazi hizo, wafundishwe na wapewe kazi.

Leo imeanguka ndege ya watu 43 vipi ikianguka ile kubwa ya watu 330? Hizi ni ishara kwamba kubwa linakuja. Tuwekeze!

Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu na kuziweka mahala pema peponi. Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe.

***Ngurumo ya Mwandishi,***
***November 5.***

# MWANDISHI WETU: JULLIE A. MMASSI
## (Kusudi Halisi)

**Katika ukuta wa Mwandishi Wetu, leo tunakuletea, mama, mwalimu, mlezi. Si maarufu sana kwenye uwanja wa waandishi lakini ni mwenye ubobevu katika uga huo. Hebu mtambue halafu tafuta kazi ake kupitia maelekezo tutayokupa.**
**Yeye mwenyewe anajieleza...**



NAITWA KUSUDI HALISI.
Ni jina langu halisi kwa sasa.
Majina yangu ya zamami ni Jullie A. Mmassi.
Elimu yangu ni ya kidato cha nne.
Na ni mwalimu mstaafu wa daraja la 111 A

Nilianza uandishi tangu mwaka 1999, ila niliandika Riwaya zangu kwenye magazeti ya JITAMBUE, NIPASHE NA UHURU.
Nilitamani sana kufundisha kwa njia ya uandishi kuhusu maisha na yale yote yanayotuzunguka katika maisha. Nikiwa nimechochewa sana na shangazi yangu ambaye alikuwa anatufundisha kupitia hadithi.

Mpaka sasa nimefanikiwa kuchapisha kitabu kimoja kiitwacho **" LOLITA NAGUBIGWA NA MACHOZI."**
Lakini pia nina vitabu vingine zaidi ambavyo nimeshaviandika japo ni bado kuchapwa. Navyo ni ;

1. PIGO LA MAISHA. ( Tamthilia ).
2. USHANGA. ( Riwaya )
3. LAITI NINGEJUA. ( Riwaya )
4. KISASI CHA MAUTI ( Riwaya.)
5. NYOTE NI WAZAZI WANGU. ( Riwaya.)
6. MASKINI NDOA YANGU ( Riwaya. )
7. NAJUTA
8. KIZUKA
9. BINTI TAJIRI
10. LOLITA

Halafu kuna hadithi fupi

1. MASIKINI MIE
2. KUBALI YAISHE
3. AMUA MOJA
4. NIFICHIE SIRI
5. MKUKI KWA NGURUWE
6. HUKUMU
7. KIKULACHO

Waandishi wanaonivutia kwa hapa Tanzania ni EDGA MBOGO, ERIC SHIGONGO NA PATRIC CK

Napenda kuwaambia wasomaji kuwa wamechagua lililo jema, kwa sababu riwaya zinagusa maisha yetu ya kila siku.

Nikitolea mfano mimi mwenyewe, shangazi yetu alitufundisha mambo mengi kupitia hadithi na simulizi.

Mfano pale alipotaka kijana awe shujaa alisimulia hadithi ya kijana aliyeweza kufaulu jambo fulani kwa sababu ya ushujaa wake. Wapo waliojikuta wakipewa ufalme kwa kumuoa Binti Mfalme baada ya kupata ushindi wa kishujaa katika jambo fulani.
Hivyo tunajifunza na kuburudika pia. Tuwazoweshe watoto wetu mazoea ya kusoma vitabu tangu wakiwa wadogo.
Kitabu changu cha **Lolita Nagubikwa Na Machozi** kinapatikana Ubungo kwa Madam Sofi.
Mtafute kwa namba **0693 825 252**

Ama kweli Jungu kuu, halikosi ukoko. Kitabu cha Lolita Nagubikwa na Machozi kinahusu nini?

Riwaya hii inasimulia maisha ya msichana Lolita na familia yake iliyokuwa na maisha ya wastani. Baada ya kufanyiwa hila wakajikuta kwenye Umasikini wa kutisha. Hali hii inamfanya Lolita achukie umasikini hasa baada ya kujua tofauti iliyopo kati ya wenyenacho na wasionacho.

Lolita aliamini kupitia elimu wangeweza kujikwamua na umasikini huo. Je watafanikiwa?

Hebu kamata nakala ya kitabu hiki **'Lolita Nagubikwa na Machozi'** upate majibu.

**Ni Shilingi 15,000/= tu**

*RRM*

Penda kusoma vitabu

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

## NEW IN TOWN: 20 KALI ZA NINJA KAISAL ALLY

SIJAJUA kwanini anaitwa Kaisal! Maana Kaisal ni cheo cha watu hatari sana duniani.

Hata hivyo si nia yangu kuuliza au kujua. Leo katika *New in Town* nilitaka nikwambie tu kuwa ujio wa jarida la 20 KALI ZA NINJA KAISAL ALLY umetikisa jiji na kona zake.

Tunapozungumzia ubunifu, basi huu ndiyo haswa. Huyu jamaa ni balaa sana kwenye maswala ya uchambuzi wa filamu. Ana uwezo mkubwa wa kukusimulia mpaka we mwenyewe ukaitafuta hiyo filamu ili ujionee.

Mwezi wa kumi yaani uliopita alitoa jarida lake la uchambuzi wa filamu toleo la kwanza. Na siku hiyo ya kwanza ambayo naweza kuita ilikuwa uzinduzi aliwaalika wapenda filamu na kufanya uchambuzi huo LIVE pale Manzese.

Mmoja wa walioliandaa tukio hilo anasema, 'Nimefurahi kukutana na watu ambao nilikuwa tu nikiwafahamu mtandaoni. Nikaishuhudia maana halisi ya upendo kupitia vitendo. Watu walijaa!'




## YALIYOJIRI KWENYE MAONESHO YA VITABU YA KIMATAIFA

**Na. Mwandishi wetu**

Maonesho ya 31 ya vitabu ya kimataifa yaliyofanyika Dar es salaam mwezi Oktoba yameacha funzo kubwa kwa wapenda vitabu, watunzi na wauzaji.

Maonesho hayo yaliyowakutanisha wadau mbalimbali wa sekta hiyo katika viwanja vya Posta Kijitonyama yalipendezeshwa kwa mabanda mbalimbali ya wafanyabiashara wakubwa wa vitabu.

Sehemu maalum ya usomaji vitabu kwa watoto ilijazwa na wanafunzi wa shule za msingi waliofuatana na waalimu wao. Wanafunzi hao walioкuwa wakisoma na kucheza walikuwa ni moja ya kivutio mahali hapo.

Wapenzi wa vitabu walipata nafasi pia ya kukutana na waandishi nguli kama Shaffi Adam Shaffi mwandishi wa kitabu cha Vuta N'kuvute na wengineo katika kipengele cha *'meet the author'*.

Pia kulikuwepo hema maalum kwa ajili ya semina na warsha mbalimbali ambapo moja wapo ilikuwa ni mazungumzo ya kiuandishi yaliyowakutanisha wasomaji na wapenzi wa vitabu mbele ya waandishi Hussein Tuwa mwandishi wa Mkimbizi, Bondia, Miss Tanzania na vinginevyo. Pamoja naye Balozi Liundi mwandishi wa Samaki Nchanga, Mara Yangu ya Kwanza na vinginevyo.

'Fikra zetu tuziandike, ili kuwawekea wengine. Kitabu hakihamishiki' alisema Balozi Liundi ambaye licha ya kuelezea kuhusu vitabu vyake pia alieleza jinsi alivyoibua mawazo hayo akiwa mtumishi wa serikali.

Hussein Tuwa licha ya kuelezea kuhusu maandishi yake pia aliwaelezea washiriki namba bora ya kuweka mikakati ili kuwavuta wasomaji. 'Andika kwa njia yoyote ile, kitu kilichoandikwa huwezi kukisahau' alisema.

'Pambana, tumia mitandao ya kijamii, tumia warembo…' aliongeza kusema kwenye kukazia jinsi ya kuwavuta wasomaji.

Maoni kutoka kwa wadau mbalimbali yaliomba kuboreshwa zaidi kwa tamasha hilo hasa upande wa matangazo na upangaji wa siku za tukio. Wengi walisema hayo kutokana na idadi ndogo ya washiriki kubanwa na kazi ukizingatia zilikuwa siku za katikati ya wiki.

'Soma Vitabu Kupata Maarifa na Kujifunza'

# KITABU: MWIMBULA—Frank Masai



**Na Salum Makamba**

MWIMBULA: Kutoka kwa Mwandishi wa Watu

Kalamu itemayo wino wa dhahabu inatabaruku kwa kuangazia mila na desturi za Mwafrika kisha inahamia katika maisha ya kisasa ambayo kwa kiasi kikubwa yanaongozwa na ukuaji wa Sayansi na Teknolojia pamoja na dini.

Kalamu inagusia kwa mifano inayopumua (hai) namna Sayansi na Teknolojia inavyozipaka tope mila na desturi za Mwafrika. Kwa hekima kubwa, kalamu inaikwepa dini. Nadhani ni kwa sababu inatambua wengi wetu tulivyolowea kwenye imani. Hatusikii wala hatuambiwi. Kalamu inatuacha tulivyo. Haigusi dini hata kidogo.

Kalamu inatujuza juu ya mila na desturi ambazo zingali zinadumishwa. Upinde na Mkuki kwa kaka wa Bi. Arusi kama shukrani ya kumlinda dadaye, vitenge kwa mama na mashangazi kama ahsante kwa kumlea mke na mengineyo kedekede mithili ya manyoya kwenye mwili wa nguruwe pori.

Kalamu haichoki. Inapomaliza kutoa utangulizi huo wenye kukamata inatoa wino ambao pamoja na dhahabu yake umenakshiwa kwa machozi. Simulizi ya kusisimua iliyofumwa kwa utashi wa hali ya juu. Inayoichukua nafsi ya mwingine na kukuvisha wewe au kukuweka wewe katika mizani na mtu mwingine kisha inaketi pembeni kuona utachukua hatua gani.

Kalamu inaandika mambo ambayo si wengi hutambua kuwa yapo katika mila na desturi za Mwafrika. Kwa mfano; Eti mke wa mtu haruhusiwi kuguswa mwili wala hata kushikana mkono na mtu asiye mumewe. Ajabu! Baadhi ya watu wanaweza kudhani hapa kalamu imegusa dini. La hasha! Inaelezea mila na desturi za Mwafrika tu, ambazo wengi wanaaminishwa hazifai.

Kalamu inamwelezea binti ambaye anaziishi mila na desturi za Mwafrika alizofundwa na bibi yake. Hakuolelewa madhabahuni wala hajaunganishwa ndoani kwa viapo vizito. Heshima yake kwa mumewe inatoka moyoni. Mume awepo au asiwepo. Awe imara au dhaifu. Iwe kizani au kwenye mwanga. Anaitambua na kuitunza heshima ya mumewe.

Kalamu inainong'oneza karatasi juu ya sifa za mume wa binti. Ni mwanamume mwenye ukwasi, mashuhuri na aliyetimilizwa katika kuumbwa kwake. Binti anapitia mengi kutoka kwa ndugu wa mume huyu pamoja na mume mwenyewe (mazuri au mabaya? Sijui!) ambayo yanasokota fundo la simulizi isiyomithilika.

Kalamu inanena kwa hisia wakati ambao fundo linafumuka na kuzalisha filamu iliyokuwa mwanzo wa mageuzi na matumaini kwa mamilioni ya nafsi kote ulimwenguni (hususani za kike) zipitiazo mengi ndoani (mazuri au mabaya? Narudia tena kusema. Sijui!).

Kalamu hii inahodhiwa na kiganja cha Mwandishi Wa Watu Frank Masai. Mwenyewe amewiwa kuiita kalamu hiyo MWIMBULA.

Macho yangu yalipotazama maandiko ya dhahabu yaliyochorwa na kalamu hiyo yaliuuliza moyo, "Kaka unaona na kujifunza?" Na moyo ulikubali. Mara moja pekee haikutosha. Ikabidi nirejee mara ya pili ndipo japo nikapata nishati maungo-




ni ya kuweza kuandika japo kipande hiki kifupi kuihusu MWIMBULA.

Ukiweka mambo mengine yote katika utuo, ujumbe ulio katika kitabu hiki unatakiwa kusomwa na kueleweka vyema na kila mwanajamii. Kama wizara ingekuwa inatafuta vitabu vya kupeleka mashuleni ili kuhuisha hekima na tafakuri za vijana wa Kiafrika. Basi miongoni mwa vitabu vingi nilivyosoma mwaka huu hiki ni miongoni mwao. Nasisitiza. Kutokana na ujumbe kilioubeba.

Itafute MWIMBULA uweke ndani kwako. Isipokufaa wewe itamfaa mwingine. Hiki siyo kitabu tu. Ni ponyo na ufufuo katika maandishi.Maandishi ya kitabu hiki ipo siku yataimbwa Afrika na Duniani. Yanahitaji kufika mbali kuliko sasa na nina hakika yatafika. Aidha leo au miaka mingi ijayo.

## MAKALA: SAFARI YA NGURUMO YA MWANDISHI

### TULIKOTOKA NA TUNAKOKWENDA

Na Richard Mwambe & Rey Stanley

*Mwaka mmoja wa kazi ngumu...*

Tulikaa tukafikiri na kuona nini tunaweza kubuni ambacho kitakuwa ni sehemu ya burudani lakini pia habari kadhaa. Ila tuliona kwamba tufanye kitu cha pekee, yaani tuandike kuhusu fasihi na wanafasihi kwa ujumla.

Jambo jingine tukaona tuwatangaze au tuwasemee waandishi ambao bado wanatafuta pa kujitaangaza. Halafu tukakubaliana tutoe chapisho tepe kila mwezi tarehe 5 na tulisambaze bure kabisa. Ijapokuwa maandalizi yake yana gharama ya muda na fedha, tusijali.

Tulijua wazi kuwa kuanzisha kitu kama hiki kunahitaji majitoleo makubwa sana ya muda, akili na hata uchumi, lakini tukaona hilo si kitu, wacha tufanye. Tukafanya na naweza kusema tukafanikiwa. Mpaka sasa toleo hili la kumi na tatu, maana yake tumefunga mwaka.

Jina Ngurumo ya Mwandishi, lilibuniwa na Rey Stanley kati ya majina matatu yaliyobuniwa. Kisha likapitishwa na kazi ikaanza. Tulianza Oktoba mwaka 2021 kwa jarida lenye kurasa chache sana. Hatukuwa tunajaribu, bali tuliamua kufanya. Na kuna jambo tulililongea kwa siri sisi wawili, matokeo yake tumeyaona kwamba Ngurumo ya Mwandishi, limefungua milango ya ubunifu wa majarida kama hili.

Sasa kuna majarida kama matatu hivi na naamini mengine yanakuja. Ubunifu wa kigrafiki, uundaji wa makala, uchaguzi wa yanayotakiwa kuwemo ndipo sanaa inapolala. Na hakika kila aliyefanya jarida ameonesha umahiri wake. Kongole nyingi kwa wote. Usambazaji wetu wa kimtandao umelifikisha maili nyingi duniani, kwa kila mlumbi wa Kiswahili, na naamini linaendelea kupasua anga.

Tumepokea mirejesho toka Italia, Uingereza, Marekani, Oman, Afrika Kusini, Burundi, Kenya, Uganda na tunaamini bado tutaendelea kupokea mingine. Lakini pia kutoka hapa nchini, tumepokea na tunaendelea kupokea, pongezi, ushauri, majitoleo na kadhalika.

Yote juu ya yote tunapenda kukushukuruni ninyi nyote kwa kuwa mnalisambaza jarida hili mpaka nje ya mipaka ya bara letu. Ni ninyi mnaofanya kazi hiyo bila malipo. Ni ninyi mnaotupatia mambo mbalimbali ya kuweka jaridani. Hizi shukrani zikufikieni wapenzi wa Ngurumo ya Mwandishi.

Sasa tupo kwenye mchakato wa kubadili sura ya jarida hili ili liwe la kisasa zaidi na viwango vya juu. Tunaamini kuwa itawezekana kwani penye nia pana njia. Sasa tuna maombi mengi sana ya watu kutaka kufanya kazi na sisi. Tunawakaribisha nyote na kila mmoja tutamjibu na tutafanya kazi pamoja ili jarida letu liwe la kuvutia zaidi.

Kwenu waandishi wa tanzu mbalimbali za fasihi, tunakaribisha hadithi fupi, mashairi, tamthiliya, makala zihusuzo fasihi na waandishi. Kama wewe u mmoja wa watu hawa, tunakuomba uwasiliane nasi ili tuwape watu burudani.

Leo hii tunapotimiza mwaka mmoja tunachukua fursa hii kuwashukuru wote walioweka maandiko yao katika jarida letu, wote waliokubali kuhojiwa kwenye kurasa yetu ya 'Mwandishi Wetu' . Kazi zenu ndizo ambazo zimetufikisha hapa. Na tunaendelea kuzipokea. Tunawashukuru pia wasomaji na tunawaomba waendelee kusambaza jarida hili kwa nguvu zao zote.


Jambo la mwisho; tumepokea maombi mengi ya mashabiki wakiomba kuwa kwenye jarida hili kuwepo na riwaya ya Kamanda Amata ilikuongeza utamu. Na wengi wameshauri hata kama ni kulipia 500 kwa jarida wako tayari. Sawa, ombi lenu limepokelewa na tunalifanyia kazi.

Asanteni sana na tunawatakia siku njema, endeleeni kukaa nasi na kutusoma. *Happy Birthday Ngurumo ya Mwandishi*

***Ni sisi,***
***Ngurumo ya Mwandishi***


07

## MAKALA: SAFARI YA NGURUMO YA MWANDISHI



































**NAKALA ZETU**
**Kama hujapata za nyuma…**
**Wasiliana nasi**
**Whatsapp:**

**+255 734 514 550**
**Piga:**
**+255 766974865**

# HADITHI: USIWE MUUAJI—07 Na Jane Davis



***Ilipoishia…***

**"Fumbuka wewe mwanamke lengo langu nije nikuonyeshe madawa anayopakwa mwanao, nadhani umeamini Sasa. Tunza hayo madawa kesho mapema takupitia twende kwa mtaalamu tumdhibiti huyu mchawi kabla hajawamaliza"Aliongea Bi Stumai akaanza kupiga hatua kuondoka pale Kwa mama Masanja.**

***Endelea***

"Mmmh makubwa"
Mama Masanja alitia shaka huku akipiga viganja vyake vya mikono. Alitazama upande alikoelekea Bi Stumai ambaye tayari alikuwa kapotelea nje.

*Lakini haya mafuta mbona kama ni mafuta ya karafuu na ninavyojua hayana madhara. Sasa hiyo kesho sijui niende au vipi, ila ngoja nikubali tu kwenda maana watu husema usimuamini mtu huwenda kweli huyu kijana ninayemuona mwema akawa ni mshirikina kweli,watu huficha makucha ooho!* Aliwaza mama huku akiyatizama Kwa makini mafuta hayo.

Mara akatokeza Masunga aliyekuwa chumbani mwa mgonjwa.Alitembea taratibu akasogea hadi alipoketi mama Masanja.

"Haya mafuta nilikuwa nayatafuta sana kumbe unayo mama?"Aliongea Masunga

"Kayaleta bi Stumai kasema kayaokota huko nje wapi sijui" Kwa mara ya kwanza mama Masanja alithubutu kumuongopea Masunga.

"Mbona yalikuwa humo ndani chumbani mwa mgonjwa nilinunua Jana tu nilipokwenda sokoni "Aliongea Masunga akimtega mama Masanja.

"Basi itakuwa shemeji yako huyo alijisahau akavifagia vichupa hivyo"Aliongea mama Masanja.

"Sawa mama usijali wacha nirudi kwa mgonjwa "Aliongea Masunga aliinama akachukua vile vichupa viwili vya mafuta akaanza kuondoka kuelekea chumbani mwa mgonjwa.

*Hawa wanawake wana matatizo kweli!* Aliwaza Masunga akiweka vichupa vya mafuta mezani. Kijana yule alijiuliza maswali mengi yasiyokuwa na majibu, alimsikitikia sana mama Masanja kuwa na urafiki na jirani yake Bi. Stumai. Mwanamke mwenye kijicho, husda na roho mbaya huku kwa nje akijionyesha ni kondoo mwema ilhali ndani ni mbwa mwitu mkali. Alimhurumia sana Mama Masanja kwani alishaziona dalili mbaya, Bi. Stumai alikuwa akimrubuni amchukie yeye. Pindi mwanamke huyo akiongea na mama Masanja kijana huyo alisikia kila kitu akiwa kasimama wima nyuma ya pazia mlangoni mwa chumba cha mgonjwa.

*Dah, afadhali lakini kwa kuwa kayarudisha ngoja nimchue mwana!*

Aliwaza Masunga akichukua chupa ya mafuta ya karafuu akaifungua na kumimina mafuta kiasi mkononi mwake, akamfunua mgonjwa shuka akaanza kumchua taratibu hadi alipoona inatosha akampaka mafuta kisha akamfunika shuka.

Tayari usiku uliingia nyota nyingi zilionekana angani huku mwezi ukitoa nuru kuiangazia dunia. Masunga alikuwa ametoka bafuni kuoga alipita sebuleni akamkuta mke wa Masanja akiwa kajiinamia.

"Vipi Shem, chakula Cha mgonjwa tayari?"Aliuliza Masunga, sauti yake nzito ilimshtua mke wa Masanja akainua kichwa chake juu.

"Tayari nishamwandalia"Alijibu mke akiwa amepoteza uchangamfu wake wa siku zote.

Masunga alimtazama usoni kwa makini akagundua kitu tofauti machoni mwa mwanamke huyo. Macho yake yalikuwa mekundu sana mithili ya mtu aliyetoka kulia muda mfupi uliopita.

"Shemeji upo sawa kweli au unaumwa?"Akamuuliza huku akimtazama usoni.

"Siumwi, nipo sawa kabisa Shem"Alijibu mke wa Masanja akiwa anatazama pembeni.

"Sawa kaandae chakula naelekea kuvaa nikitoka tukampe chakula mgonjwa" Aliongea Masunga.

## HADITHI: USIWE MUUAJI—07 Na Jane Davis

"Acha tu nitamlisha mwenyewe"Aliongea mke wa Masanja.

"Mmh! Shem peke yako utaweza kweli?"Aliuliza Masunga.

"Usijali nitaweza, kama niliweza kumlisha kabla wewe hujaja vipi nishindwe leo?"Alijibu mke wa Masanja.

"Sawa Shem"Alijibu Masunga akitembea kuelekea chumbani mwake.

Mke wa Masanja hakujibu kitu alinyanyuka kwenye kiti akaelekea jikoni alikokuwa mama mkwe wake.

"Nimemuona katoka kuoga vipi kaingia kwa mgonjwa?"Aliuliza Mama Masanja.

"Hapana kafika hapo sebuleni ananiulizia chakula cha mgonjwa"Aliongea mke wa Masanja

"Enhee ukamwambiaje?"Aliuliza Mama Masanja.

"Nikamwambia kipo tayari"Alijibu mke wa Masanja.

"Weee nimekwambiaje lakini? Hivi unataka akamlishe yeye amuwekee na madawa maana simuamini kabisa Sasa hivi"Aliongea mama Masanja.

"Kweli kabisa mama mtu gani ananunua madawa kimyakimya na kuanza kumpakaa mgonjwa bila ruhusa yetu!"Aliongea mke wa Masanja.

"Mfyuuu! Tabia mbaya sana hiyo anajifanya daktari kumbe mhuni tu"Aliongea mama Masanja.

"Daktari wa mchongo hahaha" mke wa Masanja alikejeli huku akicheka.

"Sasa nenda umwambie chakula mgonjwa tunamlisha wenyewe "Aliongea mama Masanja.

"Nimeshamwambia mbona tena nikiwa nimenuna haswa kaniudhi kweli nimelia sana kumpakaa madawa yasiyoeleweka mume wangu "Alijibu mke wa Masanja.

"Peleka chakula chake muwekee mezani, kisha tangulia chumba cha mgonjwa nami nakuja sawa"Alitoa maelekezo mama Masanja.

"Sawa mama"
Aliitikia mke wa Masanja akabeba sinia lenye sahani ya ugali na bakuli lenye mboga kwa juu vikiwa vimefunikwa na kawa.

Alitembea taratibu hadi ndani sebuleni akalitua sinia lile mezani hakusubiri kuweka maji ya kunawa wala kunywa na hata hakumuita shemeji yake akaribie mezani kwa chakula. Mwanamke huyo akaelekea chumbani mwa mgonjwa alipoingia tu alipokewa na harufu kali ya mafuta ya karafuu na habatsoda.

"Mmmh! Huyu mchawi kashampakaa tena mfyuuu!" Mke wa Masanja aliongea Kwa hasira huku akitizama mezani lakini vichupa vya mafuta havikuwepo, aliinama chini ya uvungu wa meza lakini bado hakuviona, vichupa hivyo havikuwepo kabisa chumbani humo.

Wakati huohuo mama Masanja nae aliingia humo chumbani mikononi mwake akiwa amebeba Chakula Cha mgonjwa.

"Vipi unatafuta nini tena?"Aliuliza Mama Masanja.

"Vichupa vya yale madawa kampakaa tena si unasikia harufu yake"Aliongea mke wa Masanja akinyanyuka pale chini ya meza.

"Achana nae funga huo mlango tumlishe mgonjwa"Aliongea mama Masanja. Mke wa Masanja alifanya kama alivyoambiwa na mama mkwe wake, alifunga mlango kwa komeo wakaanza kumlisha mgonjwa.

Ilikuwa kazi ngumu mno Kila walipojaribu kupitisha chakula mataya hayakufunguka. Rojo la viazi liliishia kidevuni kabla halijatiririka kushuka kifuani. Wakiwa wanaendelea kuhangaika kumlisha mgonjwa mara wanasikia mlango ukigongwa.

"Atakuwa ni Masunga huyoo"Aliongea mke wa Masanja Kwa sauti ya kunong'ona.

"Shhhh! Usiitike"Mama Masanja aliongea kwa sauti ya chini akimpa ishara mke wa Masanja asiitikie.

# HADITHI FUPI: TABIA

## Na: Nelson Ntimba

***Inaendelea..***

**Biashara! Kwa staili kama ya Moscow.**

**Lakini sio biashara yenye uhakika wa kufanikiwa sana. Utekaji nyara una kanuni nyingi na mara nyingi huwa unafeli kwa sababu zaidi ya milioni. Na kwa uzoefu wangu, urefu wa uhai wa mtu aliyetekwa nyara ni masaa 36 tu. Baadhi yao huwa wanabahatika wanaachiwa uhai, lakini wengi wao huwa ni kuuliwa tu. Na baadhi hufa kwa mshtuko wa tukio lenyewe.**

Pesa za yule binti zilikuwa zinawanasa wahudumu kama ulimi wa kinyonga unavyonasa nzi. Na walipokuja kumhudumia hakuwafukuza. Alikuwa anakunywa chupa moja baada ya nyingine. Na bia ni bia tu. Kwahivyo muda sio mrefu lazima angeenda uwani. Tena sio mara moja. Ni mara nyingi tu. Na korido iliyokuwa inaenda uwani ilikuwa na kiza na ndefu halafu ndiko mlango wa pili wa kutokea nje ulipokuwepo.

Niliendelea kumtazama kupitia mwanga kidogo uliokuwa unamulika huku nikisikiliza mashairi ya muziki wa wale wanabendi. Na sio mimi tu niliyekuwa namwangalia. Wale mabwana wawili walikuwa wanamwangalia. Na mlinzi wake pia alikuwa anamwangalia.

Yule binti yeye alikuwa anamwangalia tu mpiga gitaa. Walikutanisha macho yao na mpiga gitaa akatabasamu kwa aibu na kuinama. Aliporudisha uso tena, alitabasamu tabasamu pana.

Yule binti alinyanyuka. Alijivuta nyuma ya kiti na kuanza kuelekea ilipokuwa korido itakayomuongoza hadi uwani. Mimi pia nilinyanyuka kutoka nilipokuwa nimekaa na kuelekea huko pia. Kwa hatua nilizokuwa napiga nilifika huko wa kwanza. Sauti ya muziki ilikuwa kubwa bado. Choo cha wanawake kilikuwa katikati ya korido. Cha wanaume kilikuwa kwa mbele zaidi. Niliegemea ukuta na kumwangalia yule binti akija nilipokuwa. Alikuwa amevaa viatu vya visigino virefu na suruali ya kubana na kila hatua ya mguu aliyonyanyua ilikuwa fupi tu na alitembea kawaida. Alikuwa bado hajalewa. Alikuwa ni Mrusi usisahau. Hawa watu wana vichwa vigumu. Alipofika aliusukuma mlango wa chooni na kuingia ndani.

Sekunde kumi baadae wale wanaume wawili walifika koridoni hapo. Nilihisi pengine watamsubiria atoke chooni kwanza, lakini hawakufanya hivyo. Waliniangalia tu kama vile nilikuwa ukuta wakanipuuza halafu wakaingia ndani ya choo cha wanawake. Mmoja baada ya mwingine. Mlango ukajibamiza nyuma yao. Muziki ukaendelea kulia.

Mimi niliingia baada yao. Na nikuambie tu, kila siku huwa inakuja na jambo geni. Kiukweli nilikuwa sijawahi kuingia kwenye choo chochote cha wanawake. Hii ndiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza.

Yule binti alikuwa amesimama kuegemea ukuta. Na wale wanaume walikuwa wapo mbele yake wanamtazama. Walikuwa wamenipa migongo.

Nilianza kuongea, "Oya."

Lakini hawakunisikia. Labda kwa sababu ya kelele za mziki. Hivyo niliamua kuwakamata kwenye viwiko, kila mmoja kwa mkono mmoja. Waligeuka kwa kasi wakiwa tayari kupigana, lakini ghafla wakabadili mawazo. Mimi nina mwili mkubwa na ninadhani ndicho kitu kilichowatisha. Walibaki wamesimama kwa sekunde na kuanza kuondoka. Walifungua mlango na kutoka nje.Yule binti alibaki ananitazama kwa jicho ambalo nilishindwa kutafsiri maana yake. Tulikaa hivyo bila kuongea na nikaondoka kurudi baa na kumuacha amalize shughuli yake. Niliendа kukaa kwenye meza yangu. Wale jamaa pia walikuwa wamerudi kwenye meza zao. Yule mlinzi alikuwa yupoyupo tu. Macho yake yalikuwa kwenye bendi. Na binti alikuwa bado yupo uwani.

***Inaendelea uk 13***

# ABIGAEL MWAFULILWA: MUUZA MAZIWA MSOMA VITABU



**Ana Kwa Ana, mwezi Oktoba inaniukutanisha na mwanadada Abigael. Abigael, anayejiita 'Muuza maziwa wa kishua', sikumjua kama ni mpenzi wa kusoma vitabu.**

Kwenye moja ya komenti zake *facebook* ilikuwa imelenga kwenye kile nilichoandika. Bahati iliyoje, kumbe hata sikuhitaji kusafiri kumtafuta.

Ni mkazi wa Iringa na shughuli zake afanyia hapohapo Iringa kwenye ngome ya Mtwa Mkwawa. Licha ya kusoma vitabu yeye ni msichana anayeamini kuwa nguvu na akili yake ndivyo vitavyompa maisha bora.

Tofauti na wengi wa rika lake ambao hupenda tu kujirusha na kusubiri kupewa. Na mwisho huwatokea puani.

Abigael anauza maziwa fresh na mtindi safi. Nilipomuhoji na kumchunguza zaidi aliniibia siri kuwa pia anamiliki shamba ambapo analima malimbichi na kuingiza sokoni ama hapa Iringa mjini au nje ya mkoa huu.

Tuachane na hilo, sitaki kukwambia kuhusu maisha yake. Kwanza hayanihusu!

Akanisumbua hapa na pale nimpatie kitabu. Mi siyo mchoyo na sikuzaliwa kuwa hivyo. Nikampatia kitabu kinaitwa WHO WILL CRY WHEN YOU DIE. Kisha nikamwambia 'soma, ukishasoma andika ulichojifunza!' nilichokipata sikutegemea. Alisoma na akaniorodheshea alivyojifunza.

**Mimi:** Umejifunza nini ambacho unapenda kuwaambia wenzio?

**Abigael:** Nimejifunza vitu vingi sana, cha kwanza ni kuwa mwema kwa kila mtu, cha pili kila mtu anayekuja maishani ana kitu cha kukufundisha, cha tatu kuwa na hekima ili kufurahia safari ya maisha. Vitu ni vingi mno…

Akahitaji vitabu vingine nikamwambia ninavyo vya hadithi, akanijibu.

**Abigael:** Nasoma hadithi za Kiswahili sijawahi soma za Kiingereza kabisa. Kama unavyo vya ujasiliamali ndivyo nahitaji zaidi…

Nikagundua anapenda sana vitabu vya ujasiliamali. Huyu ni mjasiliamali anayependa kujifunza mwa wengine.

**Mimi:** Usije ukasoma ukasahau kuuza maziwa

**Abigael:** Nina ratiba ya kusoma haitaingiliana na maziwa.
**Mimi:** Cashflow Quadrant umewahi kukisoma?

**Abigael:** Sijawahi nitumie maana nina mpango wa kuwa na hela *mingi*

Abigael, nimegundua, si tu msomaji wa vitabu bali ni mwenye uwezo wa kubadili kitabu kuwa maisha na ndiyo zana nzima ya Shirika letu lisilo la kiserikali la Kitabu Maisha. Siku moja nitamhoji kwa kirefu kasha nitaleta hapa kile ambacho unaweza kujifunza basi kikufae.




**Kwa wakazi wa Iringa mjini na vitongoji vyake, ABBY MILK wapo tayari kukuhudumia, kwa maziwa fresh na mtindi wenye viwango.**

**Simu: +255 627 129 136**

# MPIGA MBIO — 13



Richard Mwambe

***Ilipoishia...***

**"Asiumizwe mtu, labda kama ikibidi tu…" Kenneth akawaambia wenzake. Nao wakaitikia.**

**Vijana hawa watatu walishibana kwelikweli. Kila mmoja hakuwa na unasaba na mwenzake. Matendo yao, yaliyowafanya waingie jela ndiyo yaliyowakutanisha. Huko wakaunda urafiki, wakapanga mikakati ya kuishi pindi wakikutana uraiani. Kama serikali ilijua imewakomesa basi kumbe iliunda kirusi kingine hatari zaidi.**

***Endelea...***

Walipotoka wote, wakatafutana, wakakutana. Wakaamua kuhuisha kile walichopanga. Matajiri, wageni, ndiyo watu waliopambana nao na kuwapora pesa. Urafiki na watu nchi za Afrika Magahalibi uliwafanya wawe na uwezo wa kughushi hundi za benki kadhaa na kujichotea pesa.

Wizi huo ulijulikana, jeshi la polisi likaanza kupanga mkakati jinsi ya kuwanasa. Lilichohitaji ni utaalamu na mfanano wa alama za vidole.

Kenneth akachukua mfuko mwembamba wa plasiki na kutoa glavu inayofanana kabisa na ngozi ya binadamu akaivaa. Na wenzake wakafanya hivyo hivyo tayari kwa kazi.

Simu ya Kenneth aliita, akaiinua na kuiweka sikioni kumsikiliza huyo anayepiga.

"Nipe maelekezo!" Kenny akamwambia.

"Muindi kavaa Shati la njano na suruali nyeusi, mkoba wake una milioni kumi na saba taslim…" ile simu ikatoa maelekezo na kukatika. Kebby akaendelea kuendesha like gari mpaka jirani kabisa na ghorofa ambalo ndani yake kulikuwa na Benki kubwa ya wafanyabiashara.

"Egesha hapo!" Kenneth akamwambia Kebby huku akimpigapiga begani. "Scogon kaa chonjo!"

"Nimekusoma!" Scogon akajibu huku akiiandaa bastola yake. Dakika tano kama si sita baadae, yule mtu alitoka kwenye lile jengo na kuliendea *Land Cruiser* jeusi lililokuwa limeegeshwa kandoni tu mwa benki ile.

"Umeiona hiyo gari inayotoka?" Kenneth akauliza.

"Yap!" Kebby akajibu.

"Ifuate, hakikisha ukipata nafasi unaibana kama kawaida…" Kenny akatoa maelekezo kwa dereva wake. "Scogon unajua kazi yako…"

"Nipo gado!" Scogon akajibu. Kebby akatekeleza agizo alilopewa. Wakati lile Land Cruiser linaondoka tu na yeye akaingiza gari barabarani na kulifuata. Kutoka pale makutano ya Barabara ya Kawawa, Ally Hassan Mwinyi na Old Bagamoyo, Kebby alilifuata lile gari kupitia Barabara ya Ally Hassan Mwinyi kuelekea Daraja la Salenda. Hakuwa mbali nalo, mita chache tu nyuma baada ya kuyapita magari kadhaa yaliyomtangulia. Walipokaribia mataa ya St. Peter, Oysterbay upande wao ulisimamishwa kwa taa nyekundu.

"Bingo!" Kenneth akasema. Wakati lile *Land Cruiser* likisimama Mbele kabisa, Kebby aliliovateki gari la mbele yake kwa kudanganya kama anaelekea Masaki kisha akasimama jirani kabisa na lile gari. Kenneth akaufungua mlango na kuteremka akifuatiwa na Scogon. Walijiamini kwa kazi yao wala hawakuogopa.

Dirisha la lile *Land Cruiser* upande wa abiria lilikuwa chini. Yule Muindi alionekana wazi na lile begi likiwa kiti cha nyuma.

Scogon akazunguka kwa dereva na kumgongea kioo. Yule dereva akashusha kioo chake na kumsikiliza Scogon pasi na kujua nia yake. Scogon alimuonesha saa ya mkononi kana kwamba ni mchuuzi wa bidhaa hiyo, yule dereva alipoikodolea macho na yule muindi aligeukia upande huo. Kosa!

Scogon kwa kasi ya ajabu, aliingiza mkono ndani ya lile gari na kubofya nobu ya kufyatua loki. Zilipofunguka, Kenneth alikuwa tayari, alivuta kitasa cha mlango wa

# MPIGA MBIO — 13



nyuma, na kulivuta lile begi nje kisha akaufunga na Scogon akaminya loki na kuifunga milango yote, akatoweka.Yule dereva na Muindi walihangaika kufungua milango lakini wapi. Kebby alitia gia na kuvuka lile eneo kwa kuvunja sheria, akakunja kulia kwa mtindo was U-Turn na kurudi Morocco.

&&&&

Saa kumi jioni, askari wa lindo katika Benki ya Maendeleo ya Wazaramo walikuwa wakibadilishana zamu. Na muda huohuo wafanyakazi wa kawaida katika benki hiyo nao walikuwa wakitoka kuelekea nyumbani. Ikunda, mara tu baada ya kukanyaga ardhi ya nje alikutana na Habibu aliyekuwa anaondoka.

"Kwa hiyo msimamo wako uleule?" akamuuliza kwa sauti ya chini. Ikunda hakujibu, alimwangalia tu kwa Jicho baya, "si nakuuliza wewe!" akasisitiza. Badala ya kujibu, mwanamke huyo akatoa msonyo mrefu.

"Sawa!"Habibu akamwambia, "huwa sishindani na mwanamke, mi yangu ni matendo tu! Nakwambia hivi *show* yangu utaijua… na huyo anayekupa jeuri atanitambua vizuri…" Habibu aliongea kwa uchungu huku akipanda lile difenda lililokuja kuwachukua.

"Achana na Mimi…" Ikunda akamjibu huku akikunja kona kuelekea Makumbusho.

"Ipo siku yako!"

"Anaijua Mungu tu!" Jibu la Ikunda liliwafikia wale askari waliokuwa na Habibu garini, wakacheka. Habibu alijiinamia kwa sekunde kadhaa bila kuongea lolote. Kwa namna moja au nyingine alijisikia aibu. Donge la hasira lilimkaba kooni, akajiapia moyoni kuwa lazima amfanyie jambo mwanamke huyo. Walimpita na lile gari na kuondoka zao. Ikunda aliitoa simu yake kwenye pochi na kuanza kumpigia huyo anayemtaka. Hatua kama kumi hivi alisimama kusubiri simu ile ipokelewe. Kimya! Inaita na kukatika. Ikunda akahisi moyo kumuingia ganzi. alikuwa akimpigia Kenneth, waridi la moyo wake.

*Itaendelea*

## TABIA—inatoka uk 10

Muziki ulisimama. Au niseme ulifika mwisho. Wale wanaume wawili walisimana na kuelekea tena kule koridoni. Na watu wengine pia walianza kusimama kwaajili ya kuondoka. Nilinyanyuka nikamfuata yule mlinzi na kumgusa begani kumsontea aelewe. Lakini hakuonesha kuelewa, hadi yule dogo aliyekuwa anapiga gitaa aliponyanyuka na yule mlinzi akanyanyuka.

Hapo ndipo nikagundua nilikuwa nimekosea. Kumbe mlinzi alikuwa ni wa yule dogo mpiga gitaa na wala sio yule msichana.   Baba yake na huyu kijana alikuwa amempatia dogo wasanii wa kuimba nao kwenye jukwaa na mlinzi pamoja na dereva kwenye gari.

Na maadui wake sio watu wawili, ila watatu. Yule binti na wale wanaume wawili. Mpango makini sana.

Wangemsuburi amalize kuimba halafu wamtegeshee chooni kwa mtego wa binti na kumchukua kuondoka naye.

Niliwaacha wafanye mpango wao halafu wakati ambao yule binti alianza kumkumbatia yule dogo na kuwapa muda hawa wanaume wawili waingie bafuni ndipo nikatokea. Nilimpiga mwanaume mmoja kwa nguvu na yule wa pili nilimpiga kwa nguvu zaidi kiasi damu zikanirukia kwenye shati langu kutoka mdomoni mwake. Wale wanaume wawili walianguka chini na yule binti nilimuacha akimbie. Na muda huo ndipo mlinzi wa yule dogo aliingia chooni mule. Nilimuomba anipe shati lake. Sikutaka kutembea na shati lililojaa damu. Lingezuwa mashaka sana.

Halafu nikatoka nje ya ile baa. Kwa kawaida ingetegemewa nipite kulia, ila nilipita kushoto, ambako nilipanda treni ya 6 kutokea Bleecker kwenda Lafayette. Nilipokaa nilianza tena kuchunguza nyuso za watu waliokuwa mule. Nilianza pia kuchunguza mazingira ya mule ndani ya behewa la treni. Tabia za zamani hazipotei kirahisi.

MWISHO.

## Tangazo




Kwa maziwa bora kabisa ya mtindi usioghoshiwa, wasiliana nasi ABBYMILK tukuhudumie. Kunywa maziwa kwa afya yako.

Tunatoa huduma kwa wauzaji wote, wa jumla na rejarejaa. Unaujua mtindi OG wewe? Jaribu leo ABBYMILK

Kwa mawasiliano tupigie **+255 627 129 136**


---


Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com